JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**



Scanned with CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0757085652**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0768256129**

**Matron: 0757674297**

**Shule ya Sekondari: WANIKE**

**S.L.P. 358, NJOMBE.**

**Tarehe: 14/6/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**

**.......................................................**

**S.L.P ...........................................**

**.....................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI WANIKE HALMASHAURI YA WANGING'OMBE, MKOA NJOMBE, MWAKA 2023/2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya ............

Shule ya Sekondari WANIKE ipo umbali wa Kilometa 30 Kaskazini/Kusini/Mashariki/Magharibi mwa Mji wa Njombe Usafiri wa basi kutoka mjini Njombe unapatikana katika kituo cha mabasi Cha Njombe Nauli ni Shilingi 3500/= kwa pikipiki ni Shilingi 15,000/= na kwa bajaji ni shilingi 15,000/=



Scanned with CamScanner

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili rangi dark blue (mshono rinda box, marinda mawili kitambaa namba moja cha suti ushone mwenyewe na iwe ndefu kwa Wasichana na suruali mbili rangi dark blue zenye turn up kwa Wavulana.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
iv. Sare ya Michezo ni tisheti rangi ya zambarau na bukta rangi ya zambarau Kwa wasichana na kwa wavulana tisheti rangi nyekundu na bukta rangi nyekundu na viatu vya michezo kwa wote na pia Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta dark blue moja au zaidi
viii. Nguo za kushindia kwa wavulana suruali nyeusi yenye turn up na tisheti rangi ya kijivu Kwa wasichana sketi nyeusi rinda box kitambaa namba moja cha suti na tisheti ya kijivu na pia wote waje na track suti rangi ya blue bahari na wasije na nguo tofauti na zilizo elekezwa.
ix. Tai rangi ya dark blue
x. Tisheti (T-shirt) rangi ya blue yenye kola nyeupe na mfuko upande wa kushoto na isiwe na maandishi yoyote

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counter book kumi Q4
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro futi mbili na nusu kwa sita

vi. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Wanafunzi PGM waje na shoka moja lenye mpini na squizer moja. HGK waje na panga moja na mfagio(soft bloom), HKL waje na shoka moja na mfagio (Hard bloom)

## 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;



Scanned with CamScanner

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;



Scanned with CamScanner

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule;

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ..........................................................

**Jina la Mkuu wa Shule** RAINARD MBUNDA

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ..........................................................

MKUU WA SHULE
WANIKE S.S
S.L.P. 358
NJOMBE

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na**



Scanned with CamScanner

kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule 0757085652/0625061518
- Makamu Mkuu wa Shule 0768256129
- Mwandamizi Taaluma 0755315703/0755726808
- Mwandamizi Malezi 0766139056

SHULE YA SEKONDARI WANIKE.
FOMU YA KUKUBALI.

1. SEHEMU YA MWANAFUNZI.

A.KUJIUNGA NA SHULE HII.

Mimi ……………………………………………………………………………………………

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha tano mwaka 2023 katika shule ya sekondari wanike na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na elimu ya kujitegemea.

B.KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi ……………………………………………………………………………………………

Mwanafunzi wa kidato cha tano, tahasusi ya …………… Ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi na familia yangu kwa ujmla, kuwa sitashiriki au kuchochea fujo , mgomo na makosa ya jinai kwa muda wote niwapo shuleni na nyumbani nitakuwa raia mwema na mzalendo kwa nchi yangu.

**Saini……………………………………………… Tarehe…………………………………………**

Anuani yangu ya kudumu ni ……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………

2. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI.

Mimi ……………………………………ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari wanike mwaka 2023 na ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Aidha ninahidi nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na taifa. Na nitafuatilia maendeleo yake kitaaluma,tabia, mwenendo na nidhamu ya mtoto wangu nikishirikiana na walimu.

Anuani yangu ya kudumu ni ……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………

Namba ya simu……………………………………………………………………

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi , ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Saini ……………………………………………tarehe ……………………………………

**NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)**

Scanned with CamScanner

# MEDICAL EXAMINATION FORM.

WANIKE SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 358,
NJOMBE.
.......................

TO,
THE MEDICAL OFFICER,
..................................
..................................
..................................

Please examine...............................................................................................
As to her/his fitness for pursuing further education at this school.

a. Haemoglobin.......................................................................................................
b. P.V. bleeding.......................................................................................................
c. (i) Sight...............................................................................................................
   (ii Hearing............................................................................................................
d. Blood pressure.....................................................................................................
e. Urine for sugar and pregnancy test.......................................................................
f. Stool for routine examination...............................................................................
g. Asthma...................................................................................................................
h. Skin diseases.......................................................................
i. Leprosy..................................................................................................................
j. Epilepsy.................................................................................................................
k. Pulmonary tuberculosis...................................................................
l. Deformity...............................................................................................................
m. Mental problem....................................................................................................
n. Comments............................................................................................................

## MEDICAL CERTIFICATE.

(To be completed by the medical Officer)

I have examined the above named and consider that she /he is mentally and physically fit for studies.

Signature
.....................................................Date...........................................

Desination......................................................Station..................................
......

NB:( Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)

Scanned with CamScanner